

TANGAZO TANGAZO


Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Handeni anawatangazia wananchi wote kuwa Mh. Mkuu wa Wilaya atashiriki Kampeni ya kufanya usafi Jumamosi ya mwisho wa mwezi tarehe 26.06.2021 kuanzia saa 12.00 asubuhi hadi saa 4.00 asubuhi.

Mh. Mkuu wa Wilaya atashiriki katika Kata za Chanika kuanzi saa 12.00 Asubuhi eneo la Soko la Chanika na Mdoe kuanzia saa 2.30 asubuhi eneo la stendi Chogo. Aidha, Kata zilizobaki Wah. Madiwani watashiriki kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya. Pamoja na tangazo hilo, Mkuu wa Wilaya anaagiza Wenyeviti wote wa Mitaa wasimamie usafi katika maeneo yao. Wakati huohuo Mkuu wa Wilaya atapenda kuona **wananchi wakiendelea na usafi na biashara zao zikiwa zinaendelea kufanyika.**

Pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji anawakumbusha wananchi wa Kata za Chanika, Mdoe na Vibaoni kuwa usafi ufanyike katika maeneo yote ikiwa ni pamoja na kwenye mitaro, maeneo ya Biashara, Tasisi, Makazi, Stendi, Sokoni na maeneo ya Umma sambamba na hilo uchafu wote utakaokusanywa uwekwe kwenye mifuko au mapipa tayari kwa ajili ya kupelekwa katika Dampo la Kwenjugo kabla ya kuhitimisha zoezi la usafi.

Kata zilizobaki zifanye usafi katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kufyeka vichaka na kuokota taka zote zinazozagaa hovyoo katika Mitaa. Zoezi la usafi ni endelevu kila siku na litakuwa linahitimishwa kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

Tangazo hili limetolewa na


.....
Kenneth K. Haule
Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji
HANDENI

MKURUGENZI,
HALMASHAURI YA MJI
S. L. P 51
HANDENI